

**MAUDHUI YA TAMASHA LA KUMBUKIZI LA VITA VYA MAJIMAJI NA UTALII WA  
UTAMADUNI, TAREHE 27 FEBRUARI, 2020 MJINI SONGEA, DKT NOEL BISEKO  
LWOGA, MKURUGENZI MKUU WA MAKUMBUSHO YA TAIFA**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mr Pololet Mgema, Mkuu wa Wilaya ya Songea  
akimwakilisha Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Mrs Christina Mindeme**

**Mheshimiwa Dkt Aloyce Nzuki, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii**

**Chifu Emmanuel Zulu, Chifu wa Wangoni**

**Mtemi Fundikira kutoka Tabora**

**Mheshimiwa Odo Mwisho, Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Ruvuma**

**Mheshimiwa Abdully Msheweji, Meya Manispaa ya Songea**

**Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya**

**Viongozi wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama**

**Watumishi wa Wizara ya Maliasili na Utalii**

**Viongozi wa Vyama vya Siasa**

**Viongozi wa Dini**

**Waandishi wa Habari**

**Wageni Waalikwa**

**Mabibi na Mabwana; Itifaki Imezingatiwa**

**Habarini za Asubuhi**

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi na Wageni Waalikwa, najisikia unyenyekevu mkubwa kupewa fursa hii ya kuzungumzia maudhui ya tamasha hili muhimu la kumbukizi la vita vya majimaji.**

Leo tunakumbuka na kuenzi mashujaa wa vita vya Maji Maji ambavyo vilipiganwa takribani miaka 113 iliyopita.

Tamasha la kumbukizi la mwaka huu wa 2020 ni la 11. Kipekee kabisa, tamasha la mwaka huu limelenga **kutambua mchango wa vita vya Maji Maji katika kuendeleza na kurithisha utamaduni kwa maendeleo ta Taifa.**

Ni dhahiri kwamba vita vya Maji Maji vimebeba utajiri wa kihistoria ambao ni muhimu **kuurithisha** kwa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Kwa mfano, vita vya Maji Maji vinaonesha uzalendo, ari, ujasiri, uthubutu na umoja wa Kitaifa ambao mababu zetu walikuanao katika kutetea maslahi ya jamii dhidi ya ukoloni. Historia ya vita vya Majimaji inatukumbusha sifa za Mwafrika, inatukumbusha sisi ni nani kwa hiyo inatunza utambulisho wetu duniani. Kujitambua, uzalendo, ari, ujasiri, uthubutu na umoja ni vigezo muhimu kabisa na vya msingi vinavyohitaji **kurithishwa** kwa jamii ya sasa na ya baadaye ili kujenga jamii yenye kujiamini na kujitegemea katika nyanja mbalimbali na hasa katika nyanja ya maendeleo na uchumi, na hasa wakati huu ambapo Taifa letu linaelekea kwenye maendeleo ya uchumi wa viwanda.

Ni dhahiri pia kwamba vita vya Maji Maji vimebeba urithi wa kihistoria na kiutamaduni ambao unahitaji kufanyiwa utafiti zaidi ili kuuelewa, kuuhifadhi, na kuuendeleza kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa taifa letu. Urithi huu unaweza kuendelezwa kama chanzo cha kuvutia watalii wa ndani na nje ya nchi, na hivyo kuleta kipato – si tu kwa mtu mmoja mmoja, bali kipato kwa jamii husika na taifa kwa ujumla.

**Mheshimiwa Mgeni Rasmi na Wageni Waalikwa**, pengine – kwa kumaliza – nitambulisha tamasha hili la Maji Maji ambalo hufanyika kila mwaka hapa Songea **kama hamasa** kwa jamii zilizopo maeneo mengine ya Tanzania kuhifadhi, kurithisha na kuendeleza historia na tamaduni katika maeneo yao. Tamasha hili ni hamasa kwa wananchi kurithisha utamaduni wa kitanzania kwa Watoto katika ngazi mbalimbali, na hasa katika ngazi ya familia na mashuleni, ambapo watoto hujifunza na kujitambua wakiwa na wazazi au walezi wao nyumbani, na wakiwa na waalimu na wanafunzi wenzao mashuleni. Watoto na vijana wapewe fursa ya kutembelea makumbusho na maeneo ya kumbukumbu za kihistoria na kitamaduni ili kujifunza historia na utamaduni sahihi na kwa vitendo.

Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Makumbusho ya Taifa ipo tayari kushirikiana na jamii kutafiti, kuhifadhi, kuelimisha kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwemo mitandao, kuendeleza na kurithisha urithi wa nchi yetu kwa maendeleo ya Taifa letu.

**Kwa maneno hayo machache, na kwa unyenyekevu mkubwa kabisa, niwakaribisheni sana kwenye kilele cha tamasha la kumbukizi la vita vya Maji Maji na Utalii wa Utamaduni la mwaka 2020.**